Tafsiri imefanywa na

Paul Kisabo, Mwanasheria

0766 150 166, kisabop@gmail.com

SHERIA YA VYAMA VYA SIASA (MAREKEBISHO) YA MWAKA 2018

MPANGILIO WA VIFUNGU

SEHEMU YA I

VIFUNGU VYA AWALI

Kifungu *Jina*

1. Jina fupi

SEHEMU YA II

MAREKEBISHO YA JUMLA

2. Marekebisho ya kifungu cha 3.

3. Marekebisho ya kifungu cha 4.

4. Marekebisho ya kifungu cha 5.

5. Kuongeza kifungu kipya cha 5A na 5B.

6. Kufuta na uingizaji wa kifungu cha 6.

7. Kuongeza Sehemu mpya ya IIA.

8. Marekebisho ya kifungu cha 8.

9. Marekebisho ya kifungu cha 8A.

10. Marekebisho ya kifungu cha 8B.

11. Kuongeza kifungu cha 8C, 8D na 8E.

12. Marekebisho ya kifungu cha 9.

13. Marekebisho ya kifungu cha 10.

14. Marekebisho ya kifungu cha 10A.

15. Kuongeza kifungu cha 10B.

16. Marekebisho ya kifungu cha 11.

17. Kufuta na uingizaji wa kifungu cha 11A na 11B.

18. Marekebisho ya kifungu cha 11C.

19. Marekebisho ya kifungu cha 12.

20. Kufuta kifungu cha 12A.

21. Kuongeza kifungu cha 12C.

22. Marekebisho ya kifungu cha 13.

23. Marekebisho ya kifungu cha 15.

24. Marekebisho ya kifungu cha 18.

25. Kufuta na uingizaji wa kifungu cha 18A.

26. Marekebisho ya kifungu cha 19.

27. Kuongeza kifungu cha 19A.

28. Marekebisho ya kifungu cha 21.

29. Kufuta kifungu cha 21A.

30. Marekebisho ya kifungu cha 21B.

31. Kuongeza kifungu cha 21D na 21E.

32. Marekebisho ya kifungu cha 22.

Tafsiri ya Muswada wa marekebisho ya Sheria ya vyama vya siasa, 2018

Muswada huu utakaotolewa Bungeni umechapishwa kwa maelezo ya jumla kwa umma pamoja na taarifa ya madhumuni na sababu zake.

Dodoma, JOHN W. H. KIJAZI

Oktoba 15, 2018 Katibu wa Baraza la Mawaziri

Muswada

Kwaajili ya kutunga Sheria ili kufanya marekebisho katika Sheria ya Vyama vya Siasa,

Sura ya 258.

UMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA I

VIFUNGU VYA AWALI

Jina fupi

Sura ya 258

1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Vyama Vya Siasa (Marekebisho) ya mwaka 2018, na itasomwa kama moja na Sheria ya Vyama Vya Siasa ambayo inajulikana kama "Sheria kuu".

SEHEMU YA II

MAREKEBISHO YA JUMLA

Marekebisho ya kifungu cha 3

2. Sheria kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 3 kwa kuingiza katika safu sahihi ya alfabeti ya ufafanuzi mpya ufuatao:

"Mkutano mkuu wa chama cha siasa" maana yake ni chombo cha juu cha utawala cha chama, kilichofanywa na wajumbe wa chama kulingana na muundo wa chama uliowekwa katika katiba ya chama;

"Kamati Tendaji ya Kitaifa" maana yake ni chombo cha chama au chombo chochote kinachojumuisha viongozi wa chama na wawakilishi wa chama kutoka kila mkoa pale ambapo chama kina chombo cha kiutawala au muwakilishi aliyechaguliwa kwa mujibu wa katiba ya chama;

"Mwanzilishi wa chama cha siasa" ina maana ya mtu anayehusika katika kuundwa kwa chama cha siasa na ambaye ni miongoni mwa wanachama wa kwanza wa chama.

Marekebisho ya kifungu cha 4

3. Sheria kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 4, kwa-

(a) kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (4) yafuatayo:

"(5) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (4), kazi za ofisi ya Msajili zitakuwa-

(a) kusajili vyama vya siasa kwa mujibu wa Sheria hii na sheria nyingine yoyote iliyoandikwa;

(b) kusimamia utawala na utekelezaji wa Sheria hii;

(c) kufuatilia uchaguzi wa ndani wa chama cha siasa na mchakato wa uteuzi;

(d) kulipa na kufuatilia uwajibikaji wa ruzuku ya Serikali kwenye vyama vya siasa ambavyo vinasifa chini ya Sheria hii;

(e) kufuatilia mapato na matumizi ya vyama vya siasa na uwajibikaji wa rasilimali za chama;

(f) kutoa elimu ya kiraia kuhusu demokrasia ya vyama vingi, sheria zinazoongozwa na Msajili na mambo yanayohusiana;

(g) kusimamia elimu ya kiraia iliyotolewa kwenye vyama vya siasa;

(h) kushauri Serikali juu ya masuala yanayohusiana na vyama vya siasa na demokrasia ya vyama vingi;

(i) kuwezesha mawasiliano kati ya vyama vya siasa na Serikali;

(j) kufanya utafiti juu ya vyama vya siasa, demokrasia ya vyama vingi na kutoa fedha kwenye vyama vya siasa;

(k) kutoa sekretarieti kwenye Baraza la Vyama vya Siasa; na

(l) kufanya kazi nyingine yoyote iliyotolewa na Sheria hii au sheria nyingine yoyote iliyoandikwa.

(b) kifungu kidogo cha (5) kitasomeka kama kifungu kidogo cha (6).

Marekebisho ya kifungu cha 5

4. Sheria kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 5 kwa kufuta maneno "wasajili wasaidizi" yanayoonekana katika maelezo ya chini na yaliyomo katika kifungu cha 5 na kubadilisha neno kuwa "wakurugenzi"

Kuongeza kifungu kipya cha 5A na 5B.

5. Sheria kuu inafanyiwa marekebisho kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 5 sehemu mpya zifuatazo:

"Udhibiti wa elimu ya kiraia

5A.- (1) Mtu au taasisi iliyosajiliwa ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano inayotaka kutoa elimu ya kiraia au aina yoyote ya mafunzo ya kujenga uwezo au mpango kwenye chama cha siasa, kabla ya kufanya mafunzo hayo, kumwambia Msajili kwa maandishi lengo na aina ya mafunzo, mpango wa mafunzo, watu wanaohusika katika mafunzo hayo, vifaa vya kufundisha na matokeo yaliyotarajiwa.

(2) Baada ya kupata taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1), Msajili anaweza kukataa mpango wa mafunzo au mafunzo ya kujenga uwezo na kutoa sababu za kukataa.

(3) Mtu yeyote anayekiuka kifungu hiki, anafanya kosa na atahukumiwa kulipa faini ya shilingi milioni moja lakini si zaidi ya shillingi milioni tano au kifungo cha muda usio chini ya miezi sita lakini si zaidi ya miezi kumi na miwili au zote kwa pamoja.

(4) Taasisi yoyote ambayo inakiuka kifungu hiki, inafanya kosa na inawajika, kuhukumiwa faini ya shilingi milioni tano lakini sio zaidi ya shilingi milioni thelathini.

(5) Mtu yeyote au taasisi ambayo inakiuka kifungu hiki, pamoja na adhabu chini ya kifungu hiki itaamriwa na Msajili kuwasilisha taarifa juu ya programu ya mafunzo au mafunzo ndani ya muda ambao utatolewa na Msajili.

(6) Mtu au taasisi ambayo itashindwa kutekeleza amri chini ya kifungu cha (5) inafanya kosa.

Mamlaka ya Msajili kuhitaji taarifa kutoka kwenye vyama vya siasa

5B.- (1) Msajili, katika kutekeleza majukumu na wajibu wake chini ya Sheria hii, anaweza kutaka kutoka kwenye chama cha siasa, kiongozi au mwanachama taarifa yoyote ambayo inaweza kuhitajika kutekeleza Sheria hii.

(2) Chama cha siasa kinachokiuka kifungu hiki kitawajibika kulipa faini ya shilingi milioni moja lakini si zaidi ya shillingi milioni kumi.

(3) Mtu yeyote, akiwa mtu aliye na mamlaka juu ya chama chake cha siasa, ambaye anakiuka kifungu hiki au akitoa taarifa za uongo kwa Msajili, anafanya kosa na anastahili, kuhukumiwa faini ya shilingi milioni moja lakini si zaidi ya shilingi milioni tatu au kifungo kisichozidi miezi sita lakini si zaidi ya miezi kumi na miwili au vyote viwili.

(4) Mtu yeyote au taasisi ambayo inakiuka kifungu hiki, pamoja na adhabu chini ya kifungu hiki itaamriwa na Msajili kuwasilisha taarifa kwa muda kama ilivyoelezwa na Msajili.

(5) Msajili anaweza, ambapo chama cha siasa kinakiuka kifungu kidogo cha (4), kukisimamisha au kufuta usajili wa chama hicho cha siasa. "

Kufuta na uingizaji wa kifungu cha 6.

6. Sheria kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha 6 na kuingiza kifungu kipya kama ifuatavyo: -

"Ulinzi wa maafisa

6. Hakuna shitaka lolote litakalofunguliwa dhidi ya Msajili, Naibu Msajili, Mkurugenzi au Maafisa wengine chini ya Msajili kwa kitu chochote kilichofanywa au kilichoachwa kufanywa kwa nia njema katika kutekeleza kazi yoyote chini ya Sheria hii. "

Kuongeza sehemu mpya ya IIA

7. Sheria kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara moja baada ya Sehemu ya II sehemu mpya ifuatayo: -

"SEHEMU YA IIA

UUNDAJI WA VYAMA VYA SIASA

Uundaji wa chama cha siasa

6A.- (1) Chama cha siasa kinaweza, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Sheria hii, kuanzishwa ili kukuza malengo na madhumuni ambayo hayapo kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar au sheria yoyote iliyoandikwa katika Jamhuri ya Muungano.

(2) Chama cha siasa kitasimamiwa kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar, Sheria hii, katiba yake, kanuni za demokrasia na utawala bora, bila ubaguzi, jinsia na ushirikishwaji wa kijamii.

(3) Mkutano mkuu wa chama cha siasa na kamati tendaji ya kitaifa au chombo chochote kama hicho hakitagawa (*non delegate*) kazi zake za msingi zilizowekwa katika katiba ya chama.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo (3), kazi za msingi ina maana-

(a) katika mkutano mkuu wa kitaifa, kutunga na kurekebisha katiba ya chama; na

(b) kwa upande wa kamati ya taifa ya kiutendaji, kutunga na kurekebisha kanuni za chama.

(5) Chama cha siasa kitaendeleza umoja wa Jamhuri ya Muungano, Mapinduzi ya Zanzibar, demokrasia, utawala mzuri, kupambana na rushwa, maadili, uzalendo, mwenge wa uhuru, amani ya kitaifa na utulivu katika,

(a) uundaji na utekelezaji wa sera zake;

(b) uteuzi wa wagombea wa uchaguzi; na

(c) uchaguzi wa viongozi wake.

(6) Chama cha siasa hakitatumika kama shinikizo au kikundi cha wanaharakati.

(7) Kwa makusudi ya kifungu kidogo cha (6), kikundi cha shinikizo au kikundi cha wanaharakati kinamaanisha kundi la watu linaloshawishi maoni ya umma au hatua ya Serikali kwa sababu fulani.

Sifa za watu wanaoomba usajili wa chama cha siasa

6B. Mtu atakuwa na sifa ya kuomba usajili wa chama cha siasa kama-

(a) wazazi wote wa mtu huyo ni raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kuzaliwa;

(b) mtu huyo ni mtu mwenye akili timamu;

(c) mtu huyo hajatamkwa kufilisika na mahakama yenye mamlaka kamili;

(d) mtu huyo awe na au zaidi ya umri wa miaka ishirini na moja;

(e) mtu huyo anaweza kusoma na kuandika Kiswahili; na

(f) mtu huyo ni mtu ambaye, ndani ya miaka mitano kabla ya tarehe ya kuwasilisha maombi hakuhukumiwa au kuadhibiwa kwa kosa la uaminifu, uhalifu wa kiuchumi, rushwa au ukwepaji wa kodi.

Vikwazo katika uanachama wa chama na

ushiriki katika shughuli za vyama vya siasa

6C.- (1) Mtu atastahili kuwa mwanachama wa chama cha siasa ikiwa mtu huyo-

(a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano; na

(b) ana umri au yuko juu ya umri wa mtu mzima.

(2) Mtu hawezi kuwa mwanachama wa chama cha siasa zaidi ya kimoja.

(3) Mtu ambaye ana kadi ya uanachama wa chama cha siasa zaidi ya moja atahesabika kuwa amejiuzulu kutoka chama chake cha awali.

(4) mtu ambaye sio raia hatashiriki katika mchakato wa uamuzi wa chama cha siasa kwa lengo la kukuza malengo ya chama hicho.

(5) Mwanachama wa chama cha siasa hawezi kuondolewa kwenye chama isipokuwa taratibu zinazofaa zilizowekwa katika katiba ya chama zimezingatiwa.

(6) Mtu anayekiuka masharti ya kifungu hiki, anafanya kosa na atahukumiwa, kulipa faini ya shilingi milioni moja lakini sio zidi ya shilingi milioni tatu au kifungo kisicho chini ya kipindi cha miezi sita lakini si zaidi ya miezi kumi na miwili au vyote viwili. "

Marekebisho ya kifungu cha 8

8. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 8-

(a) katika kifungu kidogo cha 4, kwa kuingiza maneno "ambacho hakijatuma maombi ya usajili kamili" kati ya maneno "ya chama sana" na "kitamaliza muda wake"

(b) kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo (4) yafuatayo:

"(5) Usajili wa muda wa chama ambacho kimetuma maombi ya usajili kamili utakuwa halali mpaka chama kitakapopewa cheti cha usajili kamili au mpaka maombi yake ya usajili kamili yatakapokataliwa.

(6) Msajili anaweza kukataa maombi ya usajili wa chama cha siasa kama jina la chama cha siasa, kifupisho cha jina au alama yake-

(a) ni chafu au ya kuudhi;

(b) hutumiwa na chama kingine cha siasa kilichosajiliwa chini ya Sheria hii au chombo kingine chochote kilichosajiliwa chini ya sheria nyingine yoyote iliyoandikwa; au

(c) imetumiwa na chama cha siasa kilichofutiwa usajili au cheti chake cha usajili kimeisha muda wake;

(c) kifungu kidogo cha (5) kitasomeka kama kifungu kidogo cha (7). "

Marekebisho ya kifungu cha 8A

9. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 8A kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kutunga kifungu kipya kama ifuatavyo:

"(1) Kutakuwa na kuhifadhiwa na kudumishwa kumbukumbu na Msajili ambapo masuala na maelezo ya vyama vya siasa vitaingia.

(2) Kumbukumbu chini ya kifungu cha (1) zitajumuisha-

(a) kumbukumbu ya vyama vya siasa;

(b) kumbukumbu ya viongozi wa kitaifa;

(c) kumbukumbu ya wanachama wa vyama vya siasa na vyombo vya kitaifa; na

(d) kumbukumbu ya wanachama wa bodi ya wadhamini wa vyama vya siasa. "

Marekebisho ya kifungu cha 8B

10. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 8B kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) na kutunga kifungu kipya kama ifuatavyo: -

"(3) Mtu anayekiuka kifungu cha (2), anafanya kosa na atahukumiwa kulipa faini ya shilingi milioni moja lakini si zaidi ya shillingi milioni tano au kifungo kisicho chini ya kipindi cha miezi sita lakini si zaidi ya miezi kumi na miwili au vyote viwili. "

Kuongeza kifungu cha 8C, 8D na 8E.

11. Sheria kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 8B yafuatayo: -

"uzingatiaji wa daftari la usajili

8C.- (1) Kila chama cha siasa kitahifadhi orodha ya wanachama katika madaftari yaliyotengenezwa kwa-

(a) wanachama wa chama;

(b) viongozi wa chama katika kila ngazi ya utawala wa chama; na

(c) wanachama wa chombo cha chama katika kila ngazi ya utawala wa chama.

(2) Msajili anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kuhitaji chama cha siasa kuwasilisha madaftari yoyote yaliyotajwa katika kifungu cha (1) au maelezo yoyote yanayohusiana na orodha hiyo, kwa muda uliowekwa katika taarifa hiyo.

(3) Chama cha siasa ambacho kinashindwa kuzingatia mahitaji ya kifungu hiki kinaweza kusimamishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(4) Licha ya kifungu kidogo cha nne (4), kiongozi wa chama cha siasa kinachokiuka kifungu kidogo cha (1) anafanya kosa na baada ya kuhukumiwa atawajibika kulipa shilingi milioni moja na si zaidi ya shilingi milioni tatu au kifungo cha muda usio chini ya miezi mitatu lakini si Zaidi ya miezi sita au vyote viwili.

Yaliyomo katika katiba na sheria za chama cha siasa

8D.- (1) Katiba ya chama cha siasa itaeleza masuala yote yaliyotajwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Msajili, ambapo ameridhika kuwa katiba ya chama haiendani na matakwa ya Sheria hii, kwa notisi ya maandishi anaweza kukitaka chama hicho kurekebisha katiba yake ndani ya miezi sita kutoka tarehe ya taarifa ili kuhakikisha uzingatiaji.

(3) Notisi iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2) itaelezea maeneo ambayo hayajazingatiwa, namna ya marekebisho na sababu ya marekebisho hayo.

(4) Chama cha siasa kinachokiuka kifungu kidogo cha (2) kitafutiwa usajili.

Vyama vya siasa havipaswi kuunda kikundi cha ulinzi

8E.- (1) Chama cha siasa, kiongozi au mwanachama hatakiwi kuajiri, kupeleka au kuunda kikosi, kikosi cha usalama au usalama wa aina yoyote au kudumisha shirika linalotaka kufanya kazi za polisi au chombo chochote cha usalama cha serikali.

(2) Chama cha siasa hakitafanya, hakitatoa msaada wa kifedha, hakitaratibu au kutoa amri ya kufanywa au kuratibiwa, mafunzo ya aina ya kijeshi au aina yoyote ya mafunzo juu ya matumizi ya nguvu au matumizi ya silaha yoyote kwa wanachama wake au mtu mwingine yeyote yule.

(3) Chama cha kisiasa kinachokiuka mahitaji ya kifungu hiki kitafutiwa usajili na kila kiongozi au mwanachama wa chama kinachohusika atahukumiwa kifungo cha muda usiopungua miaka mitano lakini si zaidi ya miaka ishirini au vyote viwili.

Marekebisho ya kifungu cha 9

12. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 9:

(a) katika kifungu kidogo cha (1) (c), kwa kuingiza mara baada ya neno "jinsia" neno "ulemavu";

(b) katika kifungu kidogo (2) -

(i) katika maneno ya ufunguzi kwa kufuta neno "katiba" na kubadilisha kwa kuongeza maneno "katiba, sheria na"

(ii) kwa kufuta aya (f) na kuibadilisha kama ifuatavyo:

"(F) inaruhusu viongozi na wanachama wake kutamka au kutumia lugha chafu, kisasi, maneno ya kudhalilisha, kichochezi, au alama ambazo zinaweza kusababisha au kuhatarisha amani na ukosefu wa umoja wa kitaifa;

(g) hutumia au kukubali matumizi au kutetea matumizi ya dini au mashirika ya kidini ili kutimiza malengo yake. "

Marekebisho ya kifungu cha 10

13. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 10-

(a) kwa kufuta aya (b) na kubadilisha kuwa ifuatavyo:

"(B) imepata sio chini ya wanachama mia mbili ambao wenye sifa za kusajiliwa kama wapiga kura kwa madhumuni ya uchaguzi wa bunge kutoka angalau-

(i) nusu ya mikoa ya Jamhuri ya Muungano ambayo angalau mikoa miwili iko Tanzania Zanzibar kuwa mkoa mmoja kutoka Unguja na Pemba; na

(ii) mkoa mmoja ni kutoka katika kila kanda ya Tanzania Bara ambayo imetajwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii; "

Marekebisho ya kifungu cha 10A

14. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 10A kwa kuongeza mara moja baada ya aya (d) aya zingine zifuatazo:

"(E) hajatangazwa kufilisika na mahakama yenye mamlaka kamili;

Cap. 2

(f) hana sifa za kuwa katika ofisi ya umma chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano au Katiba ya Zanzibar ya 1984 au sheria nyingine yoyote iliyoandikwa. "

Kuongeza kifungu cha 10B.

15. Sheria kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 10A yafuatayo: -

"Uhakiki wa vyama vya siasa

10B.- (1) Chama cha siasa kilichosajiliwa chini ya Sheria hii, kitazingatia na kudumisha masharti ya usajili.

(2) Msajili anaweza, wakati wowote kwa notisi kamili kuthibitisha chama cha siasa ili kuhakikisha kinafuata masharti ya usajili wake. "

Marekebisho ya kifungu cha 11

16. Sheria kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 11-

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kwa kuingiza mara moja baada ya maneno "uchaguzi wa wabunge" yanayoonekana kwenye maneno "uchaguzi wa baraza la wawakilishi"

(b) katika kifungu kidogo (3), kwa kuingiza mara moja baada ya maneno "uchaguzi wa wabunge," maneno "uchaguzi wa baraza la wawakilishi"

Kufuta na uingizaji wa kifungu cha 11A na 11B.

17. Sheria kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha 11A na 11B na kutunga kifungu kipya kama ifuatavyo: -

"Vyama vya siasa kuungana

11A.- (1) Chama cha siasa kilichosajiliwa kikamilifu kwa mujibu wa Sheria hii kinaweza, ndani ya siku ishirini na moja kabla ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi mkuu, kinaweza kuungana na chama kingine kilichosajiliwa kikamilifu.

(2) Ambapo vyama vimeamua kuungana kama ilivyoandikwa chini ya kifungu kidogo cha (1), vyama vitaingia katika makubaliano kwa namna ambayo inaweza kuwa imeelezwa chini ya Sheria hii.

(3) Uamuzi wa kuungana utafanywa na mkutano mkuu wa taifa wa kila chama cha siasa kinachotaka kuungana, na itakuwa katika maandishi ili kutekelezwa kikamilifu na watu wenye mamlaka ya vyama vya siasa kutekeleza mikataba kwa niaba ya kila chama cha siasa kinachotaka kuungana.

(4) Msajili, baada ya kuridhika na yaliyomo kwenya makubaliano na kwamba vyama vimezingatia

Masharti yaliyopo ya kuungana, usajili wa muda mfupi na wa kudumu wa chama cha siasa, anaweza kusajili chama kipya kwa jina ambalo linaweza kufanywa katika makubaliano na kutoa cheti cha usajili kamili.

(5) Baada ya kusajiliwa na kutolewa cheti cha usajili kamili kwa chama kipya chini ya kifungu kidogo cha (4), Msajili atafuta usajili wa vyama vya siasa vilivyoungana na kuchapisha katika gazeti ufutwaji wa vyama vilivyoungana na usajili wa chama kipya kilichoundwa baada ya kuungana.

Ukomo wa vyama vilivyoungana

11B.- (1) Vyama vya siasa vilivyoungana kwa mujibu wa vifungu vya Sheria hii, kuanzia tarehe ya usajili wa chama kipya, vitakoma kuwepo na viongozi wote wa kisiasa waliochaguliwa, walioteuliwa au kuteuliwa kabla ya kuungana watahesabika kuwa wameachia nafasi zao za uongozi.

(2) Wanachama wa chama cha siasa ambacho kimekoma kuwepo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) wataacha kuwa wanachama wa chama hicho cha siasa na wanaweza kuwa wanachama wa chama kipya baada ya kutolewa kwa kadi ya uanachama ya chama kipya.

(3) Mali za chama cha siasa ambacho kimekoma kuwepo kwa mujibu wa kifungu hiki zitakuwa mali za chama kipya cha siasa.

(4) Neno "kiongozi wa kisiasa" kama inavyotumika katika kifungu cha (1) ina maana mtu aliyechaguliwa, aliyeteuliwa kushikilia nafasi katika ofisi ya kisiasa ikiwa ni pamoja na ofisi za rais, mbunge, mwanachama wa baraza la wawakilishi, diwani au ofisi nyingine za kisiasa ndani ya mamlaka ya serikali za mitaa ikiwa ni pamoja na mji, mtaa, kijiji na kitongoji.

Mtandao wa vyama vya siasa

11C.- (1) Vyama vya siasa vinaweza kuunda mtandao kwa kusudi la kufikia malengo ya kisiasa ya pamoja.

(2) Waziri anaweza kutunga kanuni zinazoelezea namna ya kuunda mtandao wa vyama vya siasa.

Marekebisho ya kifungu cha 11C

18. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 11C-

(a) kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha (2) yafuatayo:

"(3) Bendera ya chama haitasimamishwa katika maeneo yaliyozuiliwa na kifungu cha 12 cha Sheria hii."

(b) kwa kufuta kifungu kidogo cha (4) na kubadilisha kuwa kama ifuatavyo:

"(4) Mtu yeyote anayekiuka kifungu kidogo cha (3), anafanya kosa na atahukumiwa kulipa faini ya shilingi milioni moja lakini si zaidi ya shilingi milioni tano au kifungo cha muda usio chini ya miezi sita lakini si zaidi ya miezi kumi na miwili au vyote viwili"

(c) kfungu kidogo cha (3) na (4) kitasomeka kama kifungu cha (4) na (5) kwa mtiririko huo. "

Marekebisho ya kifungu cha 12

19. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 12-

(a) kwa kufuta kifungu kidogo (2) na kukibadilisha kuwa kama ifuatavyo: -

"(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3) mwanasiasa au mtu yeyote hatafanya shughuli ya chama, kuunda, kuanzisha au kuruhusu kuanzishwa au kuundwa katika ofisi yoyote, tawi, kitengo, vijana au shirika la wanawake au chombo kingine chochote cha siasa katika sehemu yoyote ya kazi yoyote, shuleni au sehemu nyingine ya kujifunza, maeneo ya ibada, majengo ya Serikali, taasisi za umma.";

(b) katika kifungu kidogo cha (4), kwa kufuta maneno "zaidi ya shilingi arobaini elfu" na kuyabadilisha kwa kuweka maneno "chini ya shilingi milioni moja" katikati ya maneno "faini isiyo" na maneno "au kifungo";

(c) kwa kuongeza mara moja baada ya kifungu kidogo cha (4) kifungu kidogo kipya kifuatacho:

"(5) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), chama cha siasa kinaweza kufanya kikao cha kiutawala katika maeneo yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) ikiwa maeneo hayo hutoa huduma kwa ajili ya kukodisha au malipo.

(6) Mtu hatatumia dini au taasisi ya kidini kufanikisha malengo ya chama cha siasa. "

Kufuta kifungu cha 12A.

20. Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 12A.

Kuongeza kifungu cha 12C.

21. Sheria kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 12B yafuatayo: -

"Waraka wa vyama vya siasa

12C.- (1) Chama cha siasa, ndani ya siku thelathini baada ya kupewa cheti cha usajili kamili, kitatakiwa kuwasilisha kwa Msajili waraka ulioandikwa ukiorodhesha mali zote na matumizi ikiwa ni pamoja na michango, misaada kutoka kwa wahisani, ahadi ya michango au ya misaada kutoka kwa wahisani, ikiwa ni fedha taslimu au katika aina nyingine ile, ambazo tayari au ambazo zinatarajiwa kuwa mali ya awali ya chama cha siasa na wanachama wake waanzilishi kwa mwaka wa kwanza wa kuwepo kwake.

(2) waraka uliyowasilishwa kwa Msajili chini ya kifungu kidogo cha (1)

(a) utataja vyanzo vyote vya fedha na mali nyingine za chama cha siasa; na

(b) utajumuisha maelezo mengine muhimu ambayo Msajili anaweza kuagiza.

(3) Msajili, ndani ya siku thelathini baada ya kupokea waraka unaohitajika chini ya kifungu kidogo cha (2), atatangaza waraka huo kwenye *Gazeti*

(4) Licha ya adhabu yoyote iliyotajwa na Sheria hii, Msajili atafuta usajili wa chama cha siasa ambacho-

(a) kitashindwa kuzingatia kifungu hiki; au

(b) kitawasilisha waraka ambalo ni wa uongo katika sehemu zozote za msingi."

Marekebisho ya kifungu cha 13

22. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 13-

(a) katika kifungu cha (2) kwa kuongeza mara baada ya aya (c) yafuatayo:

"(d) kutoka chanzo chochote ndani ya Jamhuri ya Muungano kama itakavyoelezwa katika kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii; "

(b) katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno "kutoka vyanzo nje ya Jamhuri ya Muungano";

(c) kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kifungu kipya kifuatacho:

"(4) Kila chama cha siasa kitaweka afisa wa hesabu kulingana na katiba yake ili kusimamia rasilimali za chama."

Marekebisho ya kifungu cha 15

23. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 15 kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kifungu kipya kifuatacho:

"(3) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), chama chochote cha siasa kinachopokea ruzuku ya Serikali kitatunza akaunti tofauti ya benki ambayo itatumika kuweka na matumizi ya ruzuku ya Serikali. "Sheria ya Vyama vya Siasa (Marekebisho)

Marekebisho ya kifungu cha 18

24. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 18 kwa kuongeza mara moja baada ya kifungu kidogo cha (5) kifungu kipya kifuatacho:

"(6) Msajili anaweza kusimamisha ruzuku kwa chama cha siasa kwa muda maalum au usiojulikana ambapo anaamini kwamba usimamizi wa chama cha siasa ambacho ni pamoja na wadhamini wake hawawezi kusimamia uwajibikaji wa fedha hizo.

(7) Chama cha kisiasa kinachopokea ripoti ya ukaguzi safi au isiyo safi kitanyimwa ruzuku inayofuata ndani ya miezi sita.

(8) Msajili anaweza, wakati wowote, ambapo hajaridhika na usimamizi wa rasilimali za chama cha siasa, atamuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum.

(9) Waziri anaweza kutunga kanuni zinazoelezea taratibu za kuzingatia ili kutekeleza vizuri masharti ya kifungu hiki. "

Kufuta na uingizaji wa kifungu cha 18A.

25. Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 18A na kutunga kifungu kipya kifuatacho:

"Uwasilishaji wa ripoti za kifedha

18A.- (1) Mwaka wa kifedha wa chama cha siasa kilichosajiliwa kikamilifu kitakuwa sawa na cha Serikali;

(2) Licha ya masharti yoyote ya Sheria hii, kila chama cha siasa-

(a) kitawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa za kifedha za akaunti zake sio Zaidi ya tarehe 30 ya mwezi Septemba wa kila kalenda ya mwaka.

(b) kitawasilisha ripoti ya ukaguzi kwa Msajili ndani ya mwezi mmoja baada ya kuwa imepokea ripoti kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. "

Marekebisho ya kifungu cha 19

26. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 19, na-

(a) kutaja yaliyomo katika kifungu cha 19 kama kifungu kidogo cha (1);

(b) kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (1) ifuatavyo:

"(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Msajili anaweza kufuta usajili wa chama cha siasa ambacho kilipata usajili kwa njia ya udanganyifu."

(c) kifungu kidogo cha (2) na (3) kitasomeka kama kifungu cha (3) na (4) kwa mtiririko huo.

Kuongeza kifungu cha 19A.

27. Sheria kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 19 kifungu kipya kifuatacho: -

"Kusimamishwa kwa usajili

19A.- (1) Msajili anaweza kusimamisha usajili wa chama cha siasa kwa idadi maalum ya siku ili kukiwezesha chama kurekebisha uvunjifu kilichoufanya kama ilivyoelezwa katika notisi iliyotolewa na Msajili.

(2) Chama cha siasa ambacho kimesimamishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) hakitakuwa na haki yoyote iliyoelezwa chini Sheria hii.

(3) Msajili atafuta usajili wa chama cha siasa ambacho kitakuwa hakijarekebisha uvunjaji kilichoufanya au kufuata Sheria kama inavyotakiwa na Msajili chini ya kifungu kidogo cha (1). "

Marekebisho ya kifungu cha 21

28. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 21 kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (2) yafuatayo:

"(3) Mtu hawezi kustahili kuwa mwanachama wa Bodi ya Wadhamini wa chama cha siasa ikiwa mtu huyo ni kiongozi wa chama."

Kufuta kifungu cha 21A.

29. Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 21A.

Marekebisho ya kifungu cha 21B.

30. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 21B-

(a) katika kifungu kidogo cha (4) kwa kufuta neno "kutoa" na kubadilisha neno hilo kuwa "kuwa"

(b) kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha (4) ifuatavyo: -

"(5) Baraza litafadhiliwa kutoka kwenye bajeti ya Serikali au fedha za wafadhili kupitia Serikali."

Kuongeza kifungu cha 21D na 21E.

31. Sheria kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 21C vifungu vipya vifuatavyo: -

"Makosa na adhabu

21D.- (1) Mtu mwenye ofisi yeyote ambaye hawezi kuzingatia maagizo au ombi la Msajili lililotolewa chini ya Sheria hii au kutoa taarifa ambayo ni ya uongo katika nyenzo yoyote au maelezo anafanya kosa.

(2) Bila kuathiri adhabu nyingine yoyote iliyotolewa katika Sheria hii, chama cha siasa kinachotoa taarifa ambayo ni ya uongo katika uhalisia, kinafanya kosa na kinastahili kuhukumiwa kwa faini si chini ya milioni kumi na si zaidi ya shilingi milioni hamsini.

(3) Mtu yeyote anayekiuka kifungu chochote cha Sheria hii ambacho hakuna adhabu maalum imetolewa, atastahili kuhukumiwa kwa faini ya shilingi milioni tatu lakini si zaidi ya shillingi milioni kumi au kifungo cha muda usio chini ya miezi sita lakini si zaidi ya mwaka mmoja au vyote.

(4) Chama chochote cha siasa ambacho kinakiuka kifungu chochote cha Sheria hii ambapo hakuna adhabu maalum imetolewa, kitahukumiwa kulipa faaini ambayo sio chini ya shilingi milioni kumi na si zaidi ya shilingi milioni hamsini au kusimamishwa au kufutiwa usajili.

Kusimamishwa kwa wanachama wa chama cha siasa

21E.- (1) Bila ya kuathiri upeo wa mamlaka yaliyotolewa na Sheria hii, Msajili anaweza kumsimamisha mwanachama yeyote wa chama cha siasa ambaye amevunja kifungu chochote cha Sheria hii kutokufanya shughuli za kisiasa.

(2) Mwanachama yeyote wa chama anayefanya shughuli za chama au za kisiasa au kushiriki katika uchaguzi au amesababisha mtu yeyote kufanya shughuli za kisiasa za chama au kushiriki katika uchaguzi kipindi ambacho chama hicho kimesimamishwa, anafanya kosa.

(3) Waziri anaweza kutunga kanuni zinazoelezea taratibu za kusimamishwa kwa wanachama wa vyama vya siasa. "

Marekebisho ya kifungu cha 22

32. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 22-

(a) kwa kufuta neno "kwa" linaloonekana mwanzoni mwa aya (d) na kubadilisha kama ifuatavyo:

"Kuelezea namna ya maandalizi ya akaunti za kifedha na namna ya"

(b) katika aya (g), kwa kuingiza maneno "yaliyotengwa na" kabla ya neno "kuhesabiwa"

(c) kwa kuingiza mara baada ya aya (j) yafuatayo:

"(K) kuelezea masuala yatakayokuwepo katika katiba ya chama;

(d) aya (k) itasomeka kama aya (l).

Dar es Saalaam, Tanzania

03.01.2019

Without prejudice

The sky has never been full occupied – Paul Kisabo